



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UAMUZI WA RUFAA ZA  
WAGOMBEA UBUNGE NA UDIWANI

Dar es Salaam, 10 Septemba, 2020

Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kikao chake cha jana tarehe 09 Septemba 2020 imepitia, imechambua na kuzifanyia uamuzi rufaa za wagombea Ubunge na Udiwani zilizowasilishwa na wagombea kupitia kwa Wasimamizi wa Uchaguzi nchi nzima.

Rufaa hizo zimewasilishwa chini ya kifungu cha 40(6) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 kikisomwa pamoja na kifungu cha 44(5) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 ambacho kinatoa fursa kwa wagombea wa Ubunge na Udiwani kukata rufaa wanapokuwa hawajaridhika na uamuzi wa Wasimamizi wa Uchaguzi kutokana na pingamizi zilizowasilishwa.

Katika kikao hicho, Tume imezipitia, kuchambua na kuzifanyia uamuzi jumla ya rufaa 67. Kati ya hizo, rufaa 22 ni za Wagombea Ubunge na 45 ni za Wagombea Udiwani.

Maamuzi ya rufaa za wagombea Ubunge ni kama ifuatavyo:-

- i. Imekubali rufaa **19** na kuwarejesha wagombea husika katika orodha ya wagombea. Rufaa hizo ni kutoka kwenye Majimbo ya Tunduru Kaskazini, Mbeya Vijijini, Songea Mjini, Karagwe, Ulanga, Chemba, Tanga, Kibamba, Nyasa, Same Mashariki, Buhigwe, Mufindi Kusini, Muheza, Tabora Kaskazini, Ubungo (2) na Kigamboni (3).
- ii. Imekataa rufaa **3** za kupinga walioteuliwa. Rufaa hizo ni kutoka kwenye Majimbo ya Kalambo, Kigamboni na Muheza.

Aidha, Tume imezipitia, kuchambua na kuzifanyia uamuzi rufaa 45 za Madiwani, kama ifuatavyo;-

- i. Imekubali rufaa **26** na kuwarejesha wagombea husika katika orodha ya wagombea Udiwani. Rufaa hizo ni kutoka kwenye Kata za Kingolwira (Morogoro Mjini), Kilakala (Morogoro Mjini), Bwera (Chato), Bugene (Karagwe Mjini), Babati (Babati Mjini), Mzingani (Tanga), Bukindo (Ukerewe), Kihanga (Karagwe), Central (Tanga Mjini), Muriti (Ukerewe), Namagondo (Ukerewe), Kakukuru (Ukerewe), Bukindo (Ukerewe), Mindu (Morogoro Mjini), Kitangiri (Ilemela), Ilemela (Ilemela), Buzuruga (Ilemela), Magaoni (Tanga), Uwanja wa Taifa (Morogoro Mjini), Kerege (Bagamoyo), Chemchem (Kondoa Mjini), Tungi (Morogoro Mjini), Ndama (Karagwe), Mbuyuni (Morogoro Mjini), Kiwanja cha Ndege (Morogoro Mjini), Igurwa (Karagwe Mjini)

- ii. Imekataa rufaa **16** za wagombea ambao hawakuteuliwa. Rufaa hizo ni kutoka kwenye Kata za Ilangala (Ukerewe), Kandawe (Magu), Mazimbu (Morogoro Mjini), Msindo (Same Magharibi), Kiomoni (Tanga Mjini), Magaoni (Tanga Mjini), Usagara (Tanga Mjini), Kayanga (Ukerewe), Namilembe (Ukerewe), Nakatunguru (Ukerewe), Bwiro (Ukerewe), Kihanga (Karagwe), Kisege (Mkuranga), Mnyajani (Tanga Mjini) na Rufaa mbili kutoka Kata ya Ngoma (Ukerewe).
- iii. Imekataa rufaa **3** za kupinga walioteuliwa. Rufaa hizo ni kutoka kwenye Kata ya Ipwani (Mbarali), Ilemela (Ilemela) na Kichangani (Ulanga).

Idadi hii inafanya jumla ya rufaa za wagombea Ubunge zilizofanyiwa uamuzi na Tume hadi sasa kufikia **111** na za wagombea Udiwani **45**. Tume itaendelea kutoa matokeo baada ya usajili na uchambuzi wa rufaa hizo. Wahusika wa rufaa hizo wameanza kujulishwa kwa barua juu ya uamuzi wa Tume.

  
Dkt. Wilson Mahera Charles

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**  
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**